

# **DINARI YA DHAHABU NA DIRHAMU YA FEDHA: UISLAMU NA HATMA YA PESA**

**Imran N. Hosein**

IMETATAFSIRIWA NA : Abdul Khamisi Akida

**MSIKITI WA JAMI'AH  
MJI WA SAN FERNANDO  
VISIWA VYA TRINIDAD NA TOBAGO**

Imechapishwa na Masjid Jami'ah,  
Mji wa San Fernando.  
Mtaa wa Mucurapo na. 76  
San Fernando.  
Visiwa vya Trinidad na Tobago

Imran N. Hosein 2007

Vitabu kadhaa vilivyoandikwa na mwandishi huyu vinapatikana bure katika  
tovuti yake: [www.imranhosein.org](http://www.imranhosein.org)

Kununua vitabu vya mwandishi huyu na na DVD za mafunzo kupitia mtandao  
vinapatikana: [www.ummahzone.com](http://www.ummahzone.com)

Vitabu na DVD pia vinapatikana kupitia kwa msambazaji:

Al-Tasneen Sdn. Bhd  
35-1, 1<sup>st</sup> Floor, Jalan Melati Utama 4  
Melati Utama Setapak,  
53100 Kuala Lumpur, Malaysia  
Simu: 603-4107 2999  
Faks: 603-4108 9815  
Barua pepe: [tasneem@streamyx.com](mailto:tasneem@streamyx.com)

Mwandishi anakaribisha maoni kuhusu kitabu hiki kupitia anuani zake za barua  
pepe: [ihosein@tsst.net.tt](mailto:ihosein@tsst.net.tt) au [inhosein@hotmail.com](mailto:inhosein@hotmail.com)

# **YALIYOMO**

Dibaji

Sura ya Kwanza:	Utangulizi
Sura ya Pili:	Pesa katika Qur'ani na Sunnah
Sura ya Tatu:	M pangilio Maalum
Sura ya Nne:	M pangilio Maalum na Ushirikiano wa Kiyahudi-Kikristo
Sura ya Tano:	Majibu Yetu
Vielelezo	

## **DIBAJI**

Nina furaha kwa kuwa kitabu hiki kimeandikwa hapa Kuala Lumpur, Malaysia, mji ambao wenyeji wake wamenionyesha wingi wa wema na ukarimu katika kipindi cha miaka kadhaa, na kimekamilishwa katika mwezi mtukufu wa Ramadhan 1428H wakati nikiwa katika mwaka wa mzunguko wa safari za hubira, nikiwa mbali na faraja za nyumbani kwangu, visiwani Trinidad.

Nikiwa kama mwandishi anayeandika kitabu huku akisafiri, kama walivyofanya wakufunzi wengi maarufu katika Uislamu katika enzi zilizopita, naguswa na kasoro ya kutoweza kupitia maktaba yangu binafsi ya nyumbani, na mara nyingi inanilazimu kuandika toka kwenye kumbukumbu. Hiyo, huenda ikasababisha makosa madogo madogo kujitokeza kutokana na usahafulifu. Naomba msamaha kwa wasomaji wangu kwa makosa yatakayojitokeza.

Ukubwa wa kitabu hiki nimeufanya uwe mdogo kwa makusudi, nikiwa na lengo la kuwapa motisha wasomaji wakipitie kwa urahisi. Lugha niliyotumia pia ni nyepesi na haina misemo ya kiufundi ya kiuchumi kama vile *pesa karatasi au noti*. Kwa hiyo basi, msomaji wa kawaida hatopata matatizo kuhusu lugha inayotumika.

Kuna uwezekano kuwa matokeo yenye kutatiza yakajitokeza katika ulimwengu wa pesa katika kipindi kifupi baada ya kuchapishwa kwa kitabu hiki, matokeo ambayo yangeongeza umuhimu wa uchambuzi uliofanywa na kuwasilishwa humu.

Pasiwe na ucheleshwaji wa kusambaza kijitabu hichi, katika lugha nyingi iwezekanavyo, ili kiwafikie Waislamu wengi iwezekanavyo katika jamii zote walipo. Kwa sababu hii, kijitabu hichi hakina masharti yoyote juu ya hati miliki. Wale, kwa upande wa pili, ambao hawakubaliani na fikra na uchambuzi uliomo humu, watajikuta wamebanwa, wakati matokeo hayo mabaya yatakapojitokeza katika ulimwengu wa pesa.

Ninalazimika kunukuu majivuno na furaha juu ya jitihada zilizofanywa na aliyekuwa mfanyakazi wa benki, Nik Mahani Mohamad, mwenye tabia ya unyenyekevu na asiye na makuu, ambaye alihusika katika jitihada za awali kutaka kuanzisha mfumo wa Benki ya Kiislamu nchini Malaysia. Aliweza kubaini misingi ya ulaghai ya zinazoitwa Benki za Kiislamu, baada ya kuhudhuria na kusikiliza hotuba yangu juu ya somo hilo katika Royal Malaysian Mint miaka michache iliyopita. Alibadilika, akabadili mwelekeo na kwa dhamira hakika, ushupavu na moyo wa kujitolea alijikita katika kupigania msimamo wa kuwepo kwa Dinari ya Dhahabu na uchumi usio na *Riba*. Yeye pamoja na mwanafunzi wangu mpendwa, Shirazuddin Adam Shah, walihusika katika kutayarisha “Mkutano wa Kimataifa wa Uchumi wa Dinari ya Dhahabu” ambao ulifanyika Kuala Lumpur, Malaysia, mwezi Julai, mwaka 2007, ambamo uchambuzi wa awali uliomo kwenye kijitabu hiki uliwakilishwa.

Namuomba Allah, mwingi wa Rehema ambariki dada Nik Mahani Mohamad kwa juhudi zake katika kurudisha Dinari za Dhahabu na uchumi usio na *Riba*. *Amin!* Na wengineo wahamasike kufuata mfano wake mwema. *Amin!*

Imran N. Hosein

Kuala Lumpur, Malaysia.

Ramadha 1428/ October 2007

# **DINARI YA DHAHABU NA DIRHAMU YA FEDHA UISLAMU NA HATIMA YA PESA**

## **SURA YA KWANZA**

### **UTANGULIZI**

Abu Bakr ibn Abi Maryam alitoa taarifa kuwa alimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu akisema: “Kwa hakika utakuja muda ambao binaadamu hawatakuwa na chochote (kilichobaki) chenye thamani isipokuwa *Dinari* (ikiwa ni sarafu ya dhahabu) na *Dirham* ( ikiwa ni sarafu ya fedha)” [Utabiri huu kwa uhakika unaashiria na kutarajia kuvunjika kwa mfumo wa kilaghai wa pesa ambao kwa sasa unatumika dunia nzima.]

(Musnad, Ahmad)

Ni jambo la kushangaza na pia la kutia aibu kuona kuwa hata wakati huu mpevu ambapo maadui wanajitayarisha kuchomea mlango wa mwisho wa chuma katika Guantanamo ya kipesa, Waislamu wengi bado hawajui ubaya wa mfumo wa pesa uliotungwa na bara la ulaya. Mmoja wao amediriki hata kumlaumu mwandishi huyu kwa kuwa na mawazo ya “ajabu” kuhusu pesa.

Inaonyesha kuwa pana uelewa mdogo juu ya umuhimu wa mfumo wa pesa uliobuniwa barani ulaya katika kuwapa maadui wa Uislamu uwezo wa kujikita kwenye kuhalalisha wizi wa mali ya binaadamu wote. Pia pana ukosefu wa kujua kwamba maadui hao wametunga mfumo wa pesa ambao umewawezesha kuwa madikteta wa kipesa kutawala dunia nzima. Wamekwishafanikiwa kuwafanya watumwa mamilioni ya Waislamu (na hata pia wasiokuwa Waislamu mionganini mwa binaadamu) kwa kuwapa ujira wa kitumwa na ufukara, wakati wakifuatilia ajenda mbaya kwa niaba ya taifa la Israeli. Kwa kweli inasikitisha kuwasikia wale ambao wanawalaumu Wapakistani na Waindonesia kwa umasikini uliokithiri Pakistani na Indonesia.

Vyombo vyta habari, hata kwenye nchi ambazo zimetangaza kuwa “Uislamu” ni dini ya taifa, vinajulikana kwa kuficha habari zote zinazohusu jambo hili muhimu. Mfano mmojawapo ulikuwa “Mkutano wa Kimataifa juu ya Uchumi wa Dinari ya Dhahabu” ambao ulifanyika Putra World Trade Center, Kuala Lumpur tarehe 24 na 25 za mwezi wa saba mwaka 2007. Hotuba murua ya ufunguzi iliyotolewa na aliyekuwa Waziri Mkuu wa Malaysia, Tun Dk. Mahathir Mohamad, ilijenga mazingira mazuri katika kuhamasisha mwanzo wa mjadala wa kina juu ya ‘pesa’. Kijitabu hiki ni upanuzi wa hotuba iliyowakilishwa ikiwa na kichwa cha habari “Maeleo juu ya kupotea kwa pesa yenye thamani ya asili” ambayo iliwakilishwa kwenye mkutano huo muda mfupi baada ya hotuba rasmi. Wasomaji huenda wangependa kutathmini kuwakilishwa kwa habari za mkutano huo kwenye magazeti ya kiingereza yanayotolewa Malaysia.

Kitu kibaya zaidi kuliko kukosekana kuwakilishwa kwa habari hii kwenye vyombo vyta habari, ni kuwa wasomi wa Kiislamu (*Ulama*) wanaonekana kuwa sawa na Waislamu wa kawaida, katika uelewa wao mdogo unaoshangaza na unaosikitisha na kutia aibu na kimya chao kuhusu mfumo huu

wa ulaghai wa pesa za kisasa. Na hata pale ambapo wanagundua kuwa kuna pana makosa ya hatari katika mfumo huu wa pesa za kisasa, wengi wao katika hiki kipindi cha kisasa wanakosa ujasiri wa kuukosoa mfumo wa pesa za karatasi zisizothibitika (*non-redeemable*) kuwa ni wa ulaghai, na hivyo, *Haram*.

Serikali zinazowatala Waislamu ndizo zinazopelekea hali kuwa ya kusikitisha kuliko chochote katika eneo hili. Aidha hazielewi hatari ya mfumo wa pesa uliopo duniani hivi sasa, na pia hawataki hata kulisikia na kulijua tatizo hili. Kinachosababisha hali hiyo, ni ukweli kuwa inawabidi kuwa vibaraka wakiwa kama serikali katika kulinda uhusiano wao na shirikisho la Kiyahudi-Kikristo linalotawala dunia hivi sasa.

Tofauti pekee katika hali hii mbaya yenye kusikitisha imeonyeshwa na aliyekuwa Waziri Mkuu wa Malaysia, Dk. Mahathir Mohamad. Si vile tu alielewa hali ya unyonyaji wa mfumo wa pesa uliojengwa na Ustaarabu wa Mataifa ya Kimagharibi, bali pia, na ni sawa kabisa kufanya hivyo, amefanya kile ambacho Mufti wachache sana wa Kiislamu wameweza kufanya au hata kujaribu kufanya. Ametoa wito kutaka kurudishwa kwa Dinari ya Dhahabu kama mfumo mpya wa pesa na kuondoa mfumo uliopo uliojikita kwenye ulaghai wa Dola za Kimarekani, ili kuwawezeza Waislamu wajikomboe kutoka katika kukandamizwa na kunyonywa kipesa na kiuchumi.

Tunapendekeza somo hili juu ya ‘hatima ya pesa’ kwa faida ya wale wanaoamini Qur’ani kama ni neno la Mwenyezi Mungu Mmoja, na Mtume wake Muhammad (rehma na amani juu yake) kama Mtume wake wa mwisho. Tunafahamu kuwa inatubidi sit u kulielezea vyema somo hili, bali pia inatupasa kusali na kumuomba Allah, Mwingi wa Rehma aweze kuingilia kati na kuondoa mapazia mengi kutoka katika macho ya wengi. Hapo tu ndipo watakapouona

mwisho unaokuaj kwa kasi wa mfumo wa ulaghai wa pesa uliotengenezwa kujenga na kuusimamisha ‘Utumwa Mamboleo’ juu ya binaadamu. Mfumo huo umetengenezwa hasa kuwalenga wale ambao wanaupinga sirikisho la kiajabu la Kiyahudi-Kikristo ambalo kwa sasa linatawala dunia.

Hatua ya mwisho ya mgeuzo wa mfumo wao wa pesa utashuhudia kusambaa kwa pesa za *elektroniki*, ikiwa kama kito kinachong’ara kuliko vyote katika taji lao dhalili la pesa, ambazo zitachukua nafasi ya pesa za kilaghai za karatasi zinazotumika hivi sasa duniani. Kwa uhakika, hatua hii ya mwisho tayari imeshaanza kujitokeza, na wanachohitaji hawa majambazi wa pesa wa kimataifa ni mgogoro wa kimataifa (mfano: mashambulizi kwa taifa la Iran kwa kutumia silaha za nyuklia, ambayo bado hayajatokea lakini yanaweza kufanyika wakati wowote) ambayo yatasababisha kuanguka kwa Dola ya Kimarekani na kupelekeea kukimbiwa kwa mfumo mzima wa pesa zote za karatasi.

Kuanguka kwa Dola ya Kimarekani kunaonekana katika kuongezeka kwa bei ya dhahabu – ambayo kwa sasa imekaribia rekodi ya US\$850 kwa aensi moja, kwa bei ya mwezi wa kwanza 1980. Dunia inaweza kutaraji bei ya aensi moja ya dhahabu kufikia US\$3000 au hata zaidi. Hali kama hiyo pia itatokea kwenye bei ya mafuta. Huenda mshangao wa kisaikolojia utakaoikumba dunia baada ya kuanguka kwa Dola ya Kimarekani utapelekea kuzikimbia pesa za karatasi, na hivyo kupelekeea pesa za *elektroniki* kuchukua nafasi ya pesa za karatasi bila kutoka jasho, kama mfumo mpya wa pesa duniani.

Tunajaribu katika somo hili kuwakilisha kwa msomaji somo la pesa kama lilivyo katika Qur’ani Tukufu na *Sunnah* za Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*). Tunaonyesha kuwa pesa hizo (ambazo tunazziita pesa za *Sunnah*) wakati wote zilikuwa na thamani ya asili (ndani yake). Kusema hivyo, tunamaanisha kuwa, thamani ya pesa, kwa thamani yoyote iliyokuwa nayo, ukiachilia mbali mabadiliko ya thamani ambayo yanaweza kutokea kwa sababu

za kawaida za kihali, thamani ya pesa hizo siku zote ilikuwa imejihifadhi kwenye pesa zenyewe, na kwa sababu hiyo, thamani yake haikuruhusu kubadilishwa au kuamua kushushwa kwa thamani yake kiholela.

Tunaonyesha pia kuwa mfumo wa pesa uliouundwa na ushirika wa Kiyahudi-Kikristo unaotawala dunia umetengenezwa rasmi kuondoa ‘pesa zenyе thamani asilia’ kutoka katika mfumo wa pesa wa dunia na badala yake kuingiza pesa zisizokuwa na thamani ya asili. Pesa hizi za karatasi zisizothibitika zinaweza zikashushwa thamani yake. Na zikishushwa thamani, tendo hilo si vile tu linahalalisha wizi wa mali za wale wanaotumia pesa hizo, bali pia malipo ya mikopo iliyo na riba ya nchi hizo yanazidi kuwa magumu. Mwishowe nchi hizo zinanaswa kwenye mikopo isiyoweza kuilipa, na hivyo kusababisha kuwa chini ya himaya ya wale waliodhinisha kinyemela mikopo mikubwa kupita kiasi kuweza kuwa na nguvu za kuwaweka chini ya matakwa yao. (Soma John Perkins, ‘Confessions of an Economic Hit Man’

Pindi pesa inaposhushwa thamani, bei ya majumba, ujira, bidhaa na huduma katika nchi ambazo pesa zake zimeshushwa thamani zinashuka bei mara hadi mara kwa wale ambao wameunda mfumo huu wa pesa. Matokeo yake, sehemu moja ya dunia watu wanaishi maisha ya raha na starehe, wakati sehemu zilizobaki za dunia, huku pesa zao zikishushwa thamani mara kwa mara, wanalahazimika kutokwa majasho na kufanya kazi ngumu kitumwa ili kuwahifadhi majambazi katika utajiri wao, wakijipa tiketi za daima za daraja la kwanza katika meli ya maisha. Umasikini unapoongezeka katika nchi zinazokumbwa na msukosuko huo wa kushushwa thamani ya pesa zao, utoaji na upokeaji wa rushwa unakithiri. Wale ambao kiwango chao cha fikra na kutafakari ni sawa na kile cha ng’ombe wanajiuliza kwa sauti: Kwa nini nchi za Kiislamu zina rushwa iliyokithiri wakati mataifa ya Magharibi (ambayo tayari yamekwishawaibia mali zao na wanaishi kwa jasho lao) hayana rushwa kabisa.

Na pale ambapo SFK - Shirikisho la Fedha la Kimataifa (IMF) unapolazimisha kubinafsisha mali katika zile nchi ambazo pesa zake zimeshushwa thamani, majambazi hayo ndipo yanapoweza kununua visima vya mafuta na gesi, kampuni za kuzalisha umeme, kampuni za simu n.k. kwa bei ya kutupa! Bado imebaki ni mshangao kuona kuwa hugo Chavez ameugundua unyonyaji wa SFK - Shirikisho la Fedha la Kimataifa (IMF) na kusimamisha uanachama katika Shirikisho hilo, wakati Ulamaa wa Kiislamu wamebaki kimya juu ya suala hili.

Katika somo hili tunaendela kuonyesha kuwa maadui hawakuridhika tu na kuishi kwa jasho la wenzao kwa kuwanyonya kwa kutumia mfumo huo walioubuni wa pesa uliokuwa wa kunyanyasa na usio wa haki. Bali tunaonyesha pia kuwa wana ajenda pana zaidi ya kuunasa umma kipesa na hivyo kuweza kudumisha udikteta wao dunia nzima. Udikteta huo utaiwezesha hatimaye nchi ya Israel kuwa mtawala wa dunia nzima, na hivyo, kwa atakayetawala Israel kuishitua dunia nzima kwa kudai kwa ulaghai kuwa yeye ni Mtume wa kweli. Kwa uhakika atakuwa *Dajjal*, Mtume wa uongo au Anti-Christ! Tuko karibu sana na tukio hilo kiasi kwamba mwandishi huyu anadiriki kutabiri kwa uhakika kuwa watoto ambao kwa sasa wako mashulenii, wataweza kushuhudia tukio hilo ((angalia *Jerusalem katika Qur'ani*) na sura ya pili ya *Surah al-Kahf na Karne ya Kisasa*, vinapatikana kwenye tovuti: [www.imranhosein.org](http://www.imranhosein.org)))

Mtu asipoweza kuelewa ajenda kamili iliyokuwa nyuma ya mfumo wa pesa hizi za karatasi zisizothibitika, hatoweza kuyakabili rasmi na kwa kupambana na changamoto zinazoletwa na kusababishwa na mfumo huo. Hata hivyo mwandishi huyu amejaribu bila mafanikio kuwashauri wasomi, wachunguzi na waalimu wa Kiislamu umuhimu wa kielwa ajenda hiyo na dhamira zake kabla ya kufanya juhud za kuurudisha mfumo wa *Dinari* ya dhahabu kama pesa halisi.

## **SURA YA PILI**

### **PESA KATIKA QUR'ANI NA SUNNAH**

Waislamu wengi wenye mtazamo wa kidunia katika karne hii ya kisasa wanaamini kuwa dini haipaswi kuingilia na kujihusisha na maisha ya kiuchumi na kisiasa. Waislamu wa aina hiyo hawatoweza kuelezea, au hata kuelewa kisa kifuatacho katika maisha ya Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*):

Abu Sa'id al-Khudri aliripoti kuwa Bilal alimletea Mtume tende za barni, na alipoulizwa na Mtume tende hizo amezipata wapi alijibu: “Nilikuwa na tende za daraja ya chini kuliko hizi na nikazibadilia *Sa's* mbili ya hizo kwa *Sa'* moja ya hizi (za daraja ya juu)” Mtume akajibu: “Ah! Hiyo ndiyo hasa asili ya *Riba*, asili hasa ya *Riba*! Usifanye hivyo, na unapotaka kununua, uza tende kwanza kama kitendo kinachojitegemea, na kisha kiasi utakachopata kitumie baadaye kwa kununulia.”

(Bukhari, Muslim)

Tunajifunza kutoka hadithi hiyo hapo juu kuwa Mtuma Muhammad (*rehma na amani juu yake*) alizuia kubadilishana idadi zisizo sawa za ‘tende’ kwa ‘tende’. Alishutumu kubadilishana huko kuwa ni *Riba*. Wakati huo huo kuna ushahidi kuwa aliruhusu kubadilishana ‘ngamia’ kwa ‘ngamia’ kwa idadi zisizo sawa.

Yahya amenieleza kutoka kwa Malik kutoka kwa Nafi'i kuwa Abdullah ibn Umar alinunua (alibadilisha) ngamia-mpandwa wa kike kwa ngania wanne na alihakikisha kuwa atawakabidhi kwa mnunuaji ar-Rabadha.

(Muwatta, Imam malik)

Swali linajitokeza: kwanini ilikatazwa kubadilishana idadi isiyo sawa kwa tende, lakini hapakuwa na kipingamizi katika kubadilishana idadi tofauti ya ngamia?

Jibu la swali hilo, linapatikana katika Hadith muhimu sana ya Mbarikiwa Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*) inayohusu *Riba*, na inaelezea nini ni pesa katika Uislamu:

Abi Sa'id al-Khudri alimripoti kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu akisema: “Dhahabu kwa dhahabu, fedha kwa fedha, ngano kwa ngano, shayiri kwa shayiri, tende kwa tende na chumvi kwa chumvi. (Pale ambapo biashara / kubadilishana ni baina ya) bidhaa zilizo sawa, malipo yakifanyika hapo hapo, basi yejote atakayetoea zaidi au atakayedai apewe zaidi, huyo amejihuisha na *Riba*, mtoaji na mpokeaji wote wana makosa sawa”

(Sahih, Muslim)

Hadithi hii ya Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*) imedhihirisha kwa uhakika mambo matatu:

**Kwanza**, imethibitisha kuwa ‘pesa’ katika Uislamu ni aidha vyuma vya thamani kama vile dhahabu, fedha au bidhaa nyingine kama ngano, shayiri, tende na chumvi vitu ambavyo ni vyakula vya kawaida na ambavyo vinahifadhika kwa muda mrefu bila kupoteza thamani yake au kuharibika kwa kuoza. Na pale palipotokea upungufu wa sarafu za dhahabu na fedha katika soko la Madina, bidhaa kama tende, ambazo zilikuwa zikipatikana kwa wingi

sokoni, na ambazo zinahifadhika, zilitumika kama pesa. Hivyo, tunaweza kujibu swalii liloulizwa hapo juu.

Kubadilishana kwa ngamia kwa idadi isiyokuwa sawa kwa sawa iliruhusiwa kwa kuwa ngamia hawakutumika kama pesa. Kubadilishana au kuuziana idadi zisizokuwa sawa kwa tende ilibidi kukatazwe kwa kuwa, tende zilitumika kama pesa, na kuruhusu kufanya hivyo, kungeruhusu wakopeshaji wa pesa kukopesha kwa Riba<sup>1</sup>

Ikiwa kanuni inayohusu bidhaa kama tende ingetumika katika visiwa vya Java, kwa mfano, basi mchele ungeweza kutumika kama pesa pale ambapo sarafu za dhahabu na fedha zingekuwa zimeadimika sokoni. Katika visiwa vya Cuba kwa upande wa pili, sukari ingeweza kutumika kama pesa, n.k.

Baadhi ya maulamaa wa Kiislamu wanatoa hoja kuwa binaadamu wako huru kutumia hata chembe chembe za mchanga kama pesa. Kwa hiyo, hakuna kizuizi kuchapisha pesa na kuzibandikia thamani yoyote ile. Msimamo wetu ni kuwa chembe chembe za mchanga au magamba ya konokono yanayopatikana ufukoni mwa bahari haviwezi kusibu kutumika kama pesa kwenye Uislamu kufuatana na *Hadith* kwani hivyo siyo vyuma vyenye thamani au bidhaa zinazotumika kama chakula na zenye uhai wa kuhifadhika.

**Pili**, pale ambapo dhahabu, fedha, ngano, shayari, tende na chumvi mchele, sukari, n.k.) vilipotumika kama pesa, thamani ya pesa ilikuwa ‘ndani’ ya pesa yenewe na siyo ‘nje’. Hivyo, hadith imedhihirisha kuwa ‘pesa’ katika Uislamu inakuwa na thamani yake ndani ya pesa yenewe.

**Tatu**, pesa wakati wote ilikuwa mionganini mwa ‘viumbe’ vya Mwenyezi Mungu katika bidhaa ambayo imeumbwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu, vikiwa na thamani iliyowekwa na kupangwa na Mwenyezi Mungu Mwenyewe. Kwani amejieleza Yeye Mwenyewe kuwa ni *al-Razzack*, Muumbaji wa mali.

Tunaweza kuelezea pesa zilizotajwa kwenye Sunna kuwa ni:

- **vyuma vyenye thamani au bidhaa nyingine kama zilivyotajwa hapo juu,**
- **pesa zenye thamani ndani ya pesa yenye,**
- **pesa zilizo umbwa na Mwenyezi Mungu Mwenyewe zikiwa na thamani kama ilivyopangwa na Yeye Mwenyewe Mwenyezi Mungu akiwa Muumbaji wa Thamani.**

Baadhi ya Ulamaa wa Kiislamu wanaharakisha kutukumbusha kuwa *Sunnah* imegawanyika katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza ni ile iliyotufikia kutoka kwa Mtume lakini ikiwa na msingi wake katika muongozo kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Na sehemu ya pili ni ile ilyokuwa na misingi yake katika ushauri wake / mawazo yake yeye mwenyewe. Mtume mwenyewe alishauri wafuasi wake kuwa “nyinyi wenyewe mnajua vizuri zaidi kuhusu masuala yenu wenyewe ya kidunia.” Fundisho linalotokana na sehemu hii ya pili ya Sunnah ni kuwa hakuna ulazima wa kufuata *Sunnah* hizi.

Ulamaa hao wanaendelea na hoja kuwa ‘pesa’ zinaingia katika sehemu hiyo ya pili ya *Sunnah*. Kutoptaka na hiyo, wanadai, ni sawa kabisa na wala hakuna dosari yoyote kwa Waislamu kukubali na kufuata mfumo uliopo wa pesa za karatasi zisizothibitika ambazo shirikisho la Kiyahudi-Kikristo linachapisha kama pesa, na kuzibandikia thamani ya ulaghai, na hivyo wao kuwa waumbaji wa utajiri kwa kiasi kikubwa wawezavyo. Kwa kufanya hivyo, wanaweza kutumia pesa zao kununua chochote, mahali popote pale duniani. Hata hivyo, Waislamu wanapofuata mfano wao katika hiki kitendo cha kufuru

ya kuumba thamani kutoka patupu, hata begi likijazwa Rupia za Indonesia au rupi za Pakistani haliwezi hata kununua kikombe cha kahawa Manhattan.

Ulamaa hao wa Kiislamu hawajawahi kutamka kuwa mfumo uliopo wa pesa za karatasi zisizothibitika ni *Haram*, na inaonyesha kama vile hawatofanya hivyo daima. Kwa uhakika wamo kwenye makosa na itawabidi wakabili matokeo ya kukosa kukiri kwao huko Siku ya Kiyama. Hawatambui kuwa pesa katika mfumo wa vyuma vyenye thamani vilivyoumbwa na Allah vikiwa na thamani yake ndani yake kama ilivyowekwa na Mwenyezi Mungu Mwenyewe ina uthibitisho wa uhakika ndani ya Qur'ani Tukufu.

Mwenyezi Mungu Mtukufu ameitaja *Dinar* katika aya hii ya *Surah Al-Imran*

﴿ وَمِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ مَنْ إِنْ تَأْمُنَهُ بِقِنْطَارٍ يُوَدِّه إِلَيْكَ وَمِنْهُمْ مَنْ إِنْ تَأْمُنَهُ بِدِينَارٍ لَا يُوَدِّه إِلَيْكَ إِلَّا مَا دُمْتَ عَلَيْهِ قَائِمًا ذَالِكَ بِأَنَّهُمْ قَاتُلُوا إِلَيْسَ عَلَيْنَا فِي الْأُمِّيْنَ سَبِيلٌ وَيَقُولُونَ عَلَى اللَّهِ الْكَذِبُ وَهُمْ

يَعْلَمُونَ ﴾٧٥﴾

“Na mionganini mwa Watu wa Kitabu (ik. Taurat) yupo ambaye ukimpa amana ya mrundi wa mali atakurudishia, na mionganini mwao yupo ambaye ukimpa amana ya dinari moja hakurudishii isipo kuwa ukimsimamia kumdai. Haya ni kwa kuwa wakisema: Hatuna lawama kwa ajili ya hawa wasio jua kusoma. Na wanamzulia uwongo Mwenyezi Mungu, hali nao wanajua.

(Qur'ani, Al-Imran , 3:75)

Na pia ameitaja *Dirhamu* katika aya hii ya *Sura Yusuf*:

وَشَرَوْهُ شَمَنْ بِخَسِّ دَرَاهِمَ مَعْدُودَةٍ وَكَانُوا فِيهِ مِنْ  
الْزَّهْدِ يَنْتَهُونَ



“Na wakamuuza kwa thamani duni, kwa akali ya pesa (*Dirhamu*). Wala hawakuwa na haja naye.”

(Qur’ani, Yusuf, 12:20)

Kati aya hizi zote mbili za Qur’ani, Mwenyezi Mungu amezitaja ‘pesa’ kama sarafu za ‘dhahabu’ au ‘fedha.’ *Dinari* ilikuwa ni sarafu ya dhahabu ambayo yenyewe ilikuwa na thamani ndani yake, na *Dirhamu* au sarafu ya fedha, pia ilikuwa na thamani ndani ya sarafu yenyewe. Zote ni miongoni mwa alivyouumba Mwenyezi Mungu na vyote vina thamani ambayo Mwenyezi Mungu amevikadiria, akiwa kama Muumba wa mali.

Zipo aya nyingine za Qur’ani ambazo pia zinazitaja dhahabu na fedha, vikiwa kama mali, na mali hizo kuweza kutumika kama pesa zikiwa katika hali ya sarafu ya dhahabu *Dinari* na sarafu ya fedha, *Dirhamu*:

رُّزِّقَنَ لِلنَّاسِ حُبُّ الْشَّهَوَاتِ مِنَ النِّسَاءِ وَالْبَنِينَ وَالْقَنَطِيرِ  
 الْمُقْنَطِرَةِ مِنَ الْذَّهَبِ وَالْفِضَّةِ وَالْخَيْلِ الْمُسَوَّمَةِ  
 وَالْأَنْعَامِ وَالْحَرْثِ ذَلِكَ مَتَّكِعٌ الْحَيَاةُ الدُّنْيَا وَاللَّهُ عِنْدَهُ

## حُسْنُ الْمَعَابِ

“Watu wamepambiwa kupenda matamanio ya wanawake, na wana (watoto), na mirundi ya dhahabu (*Dinari*) na fedha (*Dirhamu*), na farasi asili, na mifugo, na mashamba. Hayo ni starehe ya maisha ya duniani; na kwa Mwenyezi Mungu ndio kwenye marejeo mema.”

(Qur’ani, Al-Imran, 3:14)

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا وَمَا تُؤْمِنُ بِهِمْ كُفَّارٌ فَلَنْ يُقْبَلَ مِنْ أَحَدٍ هُمْ مِلْءٌ  
 الْأَرْضِ ذَهَبًا وَلَوْ أَفْتَدَيْ بِهِ أُولَئِكَ لَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ وَمَا لَهُمْ مِنْ

## نَصْرِينَ

“Hakika wale walio kufuru, na wakafa hali ni makafiri haitakubaliwa kutoka kwa yejote wao **fidia** ya **dhahabu** ya kujaza dunia nzima lau wangeli itoa. Hao watapata adhabu chungu, wala hawatakuwa na wa kuwanusuru.”

(Qur’ani, Al-Imran, 3:91)

يَأَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِنَّ كَثِيرًا مِّنَ الْأَجْبَارِ وَالرُّهْبَانِ  
 لَيَأْكُونَ أَمْوَالَ النَّاسِ بِالْبَطْلِ وَيَصُدُّونَ عَنْ سَبِيلِ  
 اللَّهِ وَالَّذِينَ يَكْرِزُونَ كَالْذَّهَبَ وَالْفِضَّةَ وَلَا يُنْفِقُونَهَا فِي  
 سَبِيلِ اللَّهِ فَبَشِّرْهُمْ بِعِذَابٍ أَلِيمٍ

“Enyi mlio amini! Hakika wengi katika makuhani na wamonaki wanakula mali za watu kwa baat’ili na wanazuilia Njia ya Mwenyezi Mungu. Na wanao kusanya dhahabu na fedha, wala **hawazitumii** (*hii bila shaka inadhamiria matumizi ya dhahabu na fedha kama pesa*) katika Njia ya Mwenyezi Mungu, wabashirie (ewe Muhammad) khabari ya adhabu iliyo chungu.”

(Qur’ani, Al-Tawba 9:34)

وَلَوْلَا أَنْ يَكُونَ النَّاسُ أُمَّةٌ وَحِدَةٌ لَجَعَلْنَا الَّمَنَ يَكْفُرُ بِالرَّحْمَنِ  
 لِبِيُوتِهِمْ سُقْفًا مِنْ فِضَّةٍ وَمَعَارِجَ عَلَيْهَا يَظْهَرُونَ

﴿٣٢﴾

وَلِبِيُوتِهِمْ أَبْوَابًا وَسُرُّاً عَلَيْهَا يَتَكَبَّرُونَ

﴿٣٤﴾

وَزِخْرًا وَإِن كُلُّ ذَلِكَ لَمَّا مَتَّعَ الْحَيَاةَ الدُّنْيَا وَالْآخِرَةُ عِنْدَ

رَبِّكَ الْمُتَقِينَ 

“Na lau isinge kuwa watu watakuwa kundi moja tungeli wajaalia wanao mkufuru Rahmani wana nyumba zao zina dari ya fedha, na ngazi zao pia wanazo pandia, Na milango ya nyumba zao na vitanda wanavyo egemea juu yake, na mapambo (zukhruf –ik. dhahabu). Lakini hayo si chochote ila ni starehe ya maisha ya dunia tu, na Akhera iliyoko kwa Mola wako Mlezi ni ya wenyewe kumcha Mungu.”

(Qur’ani, Zukhruf, 43:33-35)

وَإِنْ أَرَدْتُمُ اسْتِبْدَالَ زَوْجَ مَحَّاكَبِ زَوْجٍ وَءَايَتِمْ إِحْدَى هُنَّ  
قِنْطَارًا فَلَا تَأْخُذُوا مِنْهُ شَيْئًا أَتَأْخُذُونَهُ بِهَتَّنَا وَإِثْمًا

 مُبِينًا

“Na mkitaka kubadilisha mke mahali pa mke, na hali mmoja wao mmempa chungu ya mali (*Qintar – ik. mali ya sarafu za dhahabu na fedha*), basi msichukue katika hayo kitu chochote. Je, mtachukua kwa dhulma na kosa lilio wazi?”

(Qur’ani, al-Nisa, 4:20)

Qur'ani inaendelea kutupa habari zisizokuwa za kawaida kuwa dhahabu na fedha zitaendelea kuwa na uzito wa thamani hata katika maisha yajayo pia. Kwa maneno mengine, dhahabu na *fedha vinabeba thamani ya kiroho ikiwa nyongeza katika thamani zao katika dunia hii ya materii*.

عَلَيْهِم مِّنْ يَابْ سُدُّنْ خُضْرٌ وَّاسْتَرِيقٌ وَّحَلَوْا أَسَاوِرَ مِنْ فِضَّةٍ وَّسَقَهُمْ  
رَبِّهِمْ شَرَابًا طَهُورًا ﴿٢١﴾

“Juu yao zipo nguo za hariri laini za kijani kibichi, na hariri nzito ya at'ilasi. Na watavikwa vikuku vya fedha, na Mola wao Mlezi atawanywesha kinywaji safi kabisa.”

(Qur'ani, Al-Insan, 76:21)

يُطَافُ عَلَيْهِم بِصِحَافٍ مِّنْ ذَهَبٍ وَّأَكْوَابٌ وَّفِيهَا مَا تَشَهَّدُ  
الْأَنْفُسُ وَتَلَذُّلُ الْأَعْيُنُ وَأَنْتُمْ فِيهَا خَلَدُونَ ﴿٢١﴾

“Watakuwa wanapitishiwa sahani za **dhahabu** na vikombe; na vitakuwamo ambavyo nafsi zinavipenda na macho yanavifurahia, na nyinyi mtakaa humo milele.”

(Qur'ani, Al-Zukhruf, 43:71)

فَلَوْلَا أُلْقِيَ عَلَيْهِ أَسْوِرَةٌ مِنْ ذَهَبٍ أَوْ جَاءَ مَعَهُ الْمَلَائِكَةُ



مُقْتَرِنٌ

“Basi mbona hakuvikwa vikuku vya **dhahabu**, au hawakuja Malaika pamoja naye wakamwandama?”

(Qur’ani, Al-Zukhruf, 43:53)

جَنَّتُ عَدْنٍ يَدْخُلُونَهَا يُحَلَّوْنَ فِيهَا مِنْ أَسَاوِرَ مِنْ ذَهَبٍ وَلُؤْلُؤًا



وَلِبَاسُهُمْ فِيهَا حَرِيرٌ

“Mabustani ya milele watayaingia. Huko watavikwa vikuku vya **dhahabu**, na lulu, na nguo zao humo ni za hariri.”

(Qur’ani, Al-Fatir 35:33)

إِنَّ اللَّهَ يُدْخِلُ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ جَنَّتٍ تَجْرِي  
مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ يُحَلَّوْنَ فِيهَا مِنْ أَسَاوِرَ مِنْ ذَهَبٍ



وَلُؤْلُؤًا وَلِبَاسُهُمْ فِيهَا حَرِيرٌ

“Hakika Mwenyezi Mungu atawaingiza walio amini na wakatenda mema katika Bustani zipitiwazo na mito kati yake. Watapambwa humo kwa mapambo ya mikononi ya **dhahabu** na lulu. Na mavazi yao humo ni hariri.”

(Qur’ani, Al-Hajj, 22:23)

أَوْلَئِكَ لَهُمْ جَنَّتُ عَدْنٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهِمُ الْأَنْهَرُ يُحَلَّوْنَ فِيهَا مِنْ  
أَسَاوِرَ مِنْ ذَهَبٍ وَلِبَسُونَ ثِيَابًا خَضْرًا مِنْ سُندُسٍ وَإِسْتَرْقَ مُثَيْكَيْنَ  
فِيهَا عَلَى الْأَرَائِكِ نِعْمَ الْثَوَابُ وَحَسِنَتْ مِرْفَقَا

﴿٣١﴾

“Hao watapata Bustani za milele, zinazo pita mito kati yake. Humo watapambwa kwa mavazi ya mikononi ya **dhahabu**, na watavaa nguo za kijani za hariri na at'ilasi, huku wakiegemea humo juu ya makochi. Ni malipo bora hayo! Na matandiko mazuri mno ya kupumzikia!”

(Qur’ani, al-Kahf, 18:31)

أَوْ يَكُونَ لَكَ بَيْتٌ مِنْ رُخْرُفٍ أَوْ تَرْقَى فِي السَّمَاءِ وَلَنْ تُؤْمِنَ  
لِرُقِيقَ حَتَّى تُنْزَلَ عَلَيْنَا كِتَابًا نَقْرُؤُهُ وَقُلْ سُبْحَانَ رَبِّي هَلْ كُنْتُ  
إِلَّا بَشَرًا رَسُولًا

﴿٩٢﴾

“Au uwe na nyumba ya **dhahabu**, au upae mbinguni. Wala hatutaamini kupaa kwako mpaka ututeremshie kitabu tukisome. Sema: Subhana Rabbi, Ametakasika Mola wangu Mlezi! Kwani mimi ni nani isipo kuwa ni mwanaadamu na Mtume?”

(Qur’ani, Al-Isra, 17:93)

Kwa uhakika, *Dinari* ya dhahabu itakuwa na nafasi kubwa sana katika Siku yenyewe ya Kiyama. Katika *Hadithi* iliyo ndefu, uzito wa wema ndani ya moyo, utakapopimwa kutumia *Dinari* ya dhahabu, utakuwa ndiyokiwango cha kupima watu gani watolewe kutoka moto wa Jehannamu. Hizi ni sentensi husika kutoka katika hadithi hiyo:

Abu-Said al-Khudri aliripoti: Siku itakapofika watu kufufliza, Mu’addhin ataaadhini: “Kila mtu afuate alichokuwa akikiabudu (aliyekuwa akimuabudu) ....”

Na watu wao watazuiliwa kwenye Moto; na watawatoa watu wengi ambao tayari wameshaanza kuzama kwenye moto hadi kufikia kati ya kiweo au kufikia kwenye magoti. Kisha watasema: “Ewe Mwenyezi Mungu hakuna tena hata mmoja aliyebak (Motoni) kufuatana na amri Yako.” Kisha Mwenyezi Mungu atasema: Rudini tena na mkawatoe (toka kwenye Moto wa Jahannamu) wale ambao kwenye mioyo yao mtakuta wema japo kiasi cha **Dinari** moja.” Nao watawatoa watu wengi kutoka Motoni. Na kisha watasema: “Ewe Mwenyezi Mungu, hatukumuacha hata mmoja baada ya kutimiza amri Yako.” Kisha Atasema:” Rudini na mkawatoe wale wote ambao katika mioyo yao mtakuta wema wa kiasi cha nusu **Dinari.**” Nao watawatoa watu wengi kutoka Motoni. Na kisha watasema: “Ewe Mwenyezi Mungu, hatukumuacha hata mmoja baada ya kutimiza amri Yako.” Kisha Atasema: Rudini na mkawatoe

wale wote ambao katika miyo yao mtakuta wema wa kiasi cha uzito wa chembe moja.” Nao watawatoa watu wengi kutoka Motoni. Na kisha watasema: “Ewe Mwenyezi Mungu, hatukumuacha hata mmoja baada ya kutimiza amri Yako na kumtoa yeyote mwenye wema wowote kwenye moyo wake....”

(Sahih Muslim)

Aya hizi za Qur’ani na Hadithi hii hapo juu inadhihirisha kuwa dhahabu na fedha ziliumbwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu zikiwa na thamani kubwa ndani yake na thamani hiyo itadumu kutoka dunia hii hafifu na itatumika tena kwenye maisha yajayo. *Aya hizo pia zinaashiria kuwa Mwenyezi Mungu, katika hekima Zake, ameumba dhahbu na fedha, zitumike, mionganini mwa mengine, kama pesa. Yeyote asiyeona hilo na ambaye anapinga ukweli huu ulio wazi, ajitayarishet kujitetea na kuutetea msimamo wake siku ya Kiyama.*

Pesa yenye thamani iliyo ndani yake leo hii imepotea kutoka katika mfumo wa pesa kote duniani. Umma wa Kiislamu dunia nzima pia una kosa la kuzisaliti na kuziacha ‘pesa’ ambazo zina msingi wake katika Qur’ani Tukufu na pesa ambayo itakuwa na thamani hata katika maisha yajayo. Waislamu tayari wameshapata pigo kubwa kwa kuziacha ‘pesa takatifu’ na kukubali badala yake mfumo wa pesa wa kilaghai wa kidunia usiokuwa na misingi yake katika Qur’ani.

Lengo letu katika somo hili ni kuelezea, kwa ufupi, kwanini na jinsi gani pesa za *Sunnah* zimetoweka. Tunawataka wale watakaosoma kijitabu hiki, waelewe na wakubaliane na hoja tunazoziwakilisha humu, na wajiwajibishe kufuatana na amri ifuatayo ya Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*):

Abu said al-Khudri alisikika akisema: Nimemsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu akisema: “yeyote kati yenu akiona (chochote kile) kibaya, basi akibadilishe kwa mkono wake, na ikiwa hawezি kufanya hivyo, basi kwa ulimi wake, na ikiwa hawezি kufanya hivyo, basi kwa moyo wake; na hyo ni hali dhaifu kuliko zote za imani.”

(Sahih, Muslim)

## **SURA YA TATU**

### **MPANGO MAALUM**

Kuna mpango maalum ambao unaunganisha siasa za kimataifa, mfumo wa kimataifa wa uchumi na dini katika dunia ya leo ya mfumo wa kiulaghai wa pesa. Maelezo yanafuata:

Kila mtoto wa Kiyahudi anajua, na anaamini kuwa, ahadi takatifu waliyopewa Wayahudi ambayo kwayo, Mwenyezi Mungu amewaaahidi kuwa historia itamalizika kwa mtu mmoja, ambaye ni Mtume na Masihi, atatawala milele dunia nzima kutokea kwenye kiti cha enzi cha David / Daud (*alaihi al-Salam*) kwenye mji mtakatifu wa Jerusalem. Kutokana na hiyo, Wayahudi wameaamini kuwa historia itaishia kwa kuwepo kwa *Pax Judaica* (Dunia iliyokuwa chini ya himaya ya Kiyahudi), na Jerusalem, kwa mara nyingine tena itakuwa kama ndiyo katikati (makao makuu) ya dunia kama ilivyokuwa wakati wa Suleyman (*alaihi al-Salam*). Wameamini kuwa *Pax Judaica* itathibitisha ukweli juu ya madai ya Wayahudi kuwa ni ya kweli, wakati huo huo itathibisha madai mengine yote yaliyobaki kuwa si ya kweli.

Ni jambo la kustaajabisha kuona kuwa Waislamu na Wakristo wote wanaungana kuamini sawa na Wayahudi kuwa historia itaisha kwa Masihi kutawala dunia kwa kufuata sheria na amani kutokea mji mtakatifu wa Jerusalem. Hata hivyo, tofauti na Wayahudi, Waislamu na Wakristo wote wanaamini kuwa Yesu, mtoto wa Bikira Maria, alikuwa Mtume Mtakatifu aliyehidiwa. Pia wote, Waislamu na Wakristo, wanaamini kuwa alichukuliwa/

alipaa mbinguni wakati alipotaka kusulubiwa na kwamba atarudi kutawala dunia tokea Jerusalem kama inavyosema ahadi Takatifu.

Qur'ani inaelezea tukio hilo la kurudi kwake, kwa kufafanua kuwa hakusulubiwa, na kuwa Mwenyezi Mungu alifanya ionekane hivyo:

وَقَوْلُهُمْ إِنَّا قَاتَلْنَا الْمَسِيحَ عِيسَى ابْنَ هَرَيْمَ رَسُولَ اللَّهِ وَمَا قَاتَلُوهُ وَمَا  
صَلَبُوهُ وَلَكِنْ شُيْءَهُ لَهُمْ وَإِنَّ الَّذِينَ أَخْتَلُفُوا فِيهِ لَفِي شَكٍّ مِّنْهُ مَا لَهُمْ  
بِهِ مِنْ عِلْمٍ إِلَّا أَيْمَاعُ الظَّنِّ وَمَا قَاتَلُوهُ يَقِينًا

157

Error!

بَلْ رَفَعَهُ اللَّهُ إِلَيْهِ وَكَانَ اللَّهُ عَزِيزًا حَكِيمًا

158

Na kwa kusema kwao: Sisi tumemuwa Masihi Isa, mwana wa Maryamu, Mtume wa Mwenyezi Mungu - nao hawakumuwa wala hawakumsalibu, bali walifananishiwa tu. Na hakika walio khitalifiana katika haya wamo katika shaka nayo. Wao hawana ujuzi nayo wowote, ila ni kufuata dhana tu. Wala hawakumuwa kwa yakini.

Bali Mwenyezi Mungu alim- tukuza (alimchukua) kwake, na hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye hikima.

(Qur'ani, al-Nisa, 4:157-158)

Wakristo wamekataa msimamo wa Qur'ani na wameendela kubaki kwenye imani yao kuwa Yesu alisulubiwa.

Wayahudi kwa upande wa pili, walimkataa Yesu kama Masihi, na wanamsubiri Masihi ambaye atakuja na kuikomboa Nchi/Ardhi Takatifu kwa ajili ya Wayahudi, atawarudisha kwenye Ardhi Takatifu na kuichukua kuwa yao, atalifufua Taifa takatifu la Kiyahudi (ik. Taifa Takatifu la Kiyahudi lillianzishwa na Mitume Daud na Suleyman), na hivyo kusababisha Israeli kuwa nchi itakayotawala dunia. Masishi huyo ataitawala dunia kutokea mji Mtakatifu wa Jerusalem kwa Pax Judaica na atarudisha Himaya ya Kiyahudi.

Kuna ushahidi wa kutosha ambao unaendelea kimaajabu ajabu *unaoonekana* kuashiria kuwa madai ya Wayahudi ni ya kweli. Hata hivyo, Ardhi Takatifu ‘ilikombolewa’ mnamo mwaka 1917. Baada ya hapo, dunia nzima ilishuhudia kurudi kwa Wayahudi kwenye Ardhi Takatifu na kuichukua kama ni mali yao, miaka 2000 baada ya kufukuzwa kutoka hapo kwa ahadi takatifu. Kuanzishwa kwa taifa la Kiyahudi kukafuatwa mwaka 1948, na mwishowe kukua kwa taifa la Israel kuwa nchi kubwa duniani kukawa wazi. Kuanzishwa kwa mfumo wa ushirikiano wa Kiyahudi-Kikristo ambayo ndiyo iliyoweka misingi ya kuanzishwa kwa ustaarabu wa mataifa ya Magharibi na imepiga hatua za kutosha kuhakikisha kuwa inaanzishwa serikali ya dunia. Hivi sasa pamebaki muda mchache sana kabla Israel haijaipiku USA kama taifa lenye nguvu kuliko mataifa yote duniani. Umebaki muda mchache sana kabla Israel haijakuwa nchi inayotawala dunia, na kiongozi wa Israel atakapojitokeza kama kiongozi wa Serikali ya dunia, kutokea Jerusalem na kuweka wazi msimamo wake kuwa yeye ni Masihi!

Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*) aliifahamisha dunia nzima kuwa Mwenyezi Mungu, ambaye ana ujuzi juu ya matokeo yote, alichukua hatua ya kumuumba Masihi wa uongo, ikiwa ni majibu na mtihani wake kwoo baada ya Wayahudi kumkataa (Masihi wake, Yesu). Mtume Muhammad ameendelea kutufahamisha kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu atamruhusu kiumbe huyo aliye mbaya na wa hatari aingie duniani katika ulimwengu ulio tofauti na ulimwengu wetu (angalia sura ya pili ya kijitabu ‘*Surah Kahf na Dunia ya Kisasa*’ yenyе kichwa cha habari ‘*Qur’ani na Wakati*’) na lengo lake litakuwa ni kujifanya Mtume wa kweli. Kwa sababu hiyo, huyo Mtume wa uongo, Dajjal atajaribu kujenga msingi ya serikali ya dunia na kuitawala dunia akiwa na makao yake Jerusalem.

Kuna habari zinazopatikana katika maisha ya Mtume Muhammad zinazoonyesha kuwa kiumbe huyo aliachiwa na kuruhusiwa aingie duniani baada ya *Hijrah* kwenda Madina, na baada ya Wayahudi wa Madina kumkataa yeye Muhammad kama Mtume wa kweli na pia kuikataa *Qur’ani* kuwa ni kitabu chenye maneno ya Mwenyezi Mungu Mtukufu yaliyoteremshwa kwa kupitia malaika Jibril. ‘*Jerusalem katika Qur’ani*’ imeielezea somo hili kwa kina zaidi.

Mtume Muhammad pia ameelezea kuwa moja ya silaha kali sana atakazotumia huyo Mtume wa uongo ili kutimiza lengo lake la kuitawala dunia akiwa na makao yake makuu Jerusalem itakuwa ni ile ya kupunguza au kuzima kabisa uwezo wa binaadamu wa kuwa na jicho la kiroho ndani ya mioyo yao, hivyo kutoweza kuona mpango wake wa udanganyifu na kuweza kuwapoteza kirahisi. (Angalia ‘*Surah Kahf na Dunia ya Kisasa*’ kwenye sura juu ya ‘*Musa na Khidr*’). Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*) ameelezea pia kuwa mpango mkali zaidi ambao Mtume wa uongo atautumia ili kuweza

kuwalazimisha binaadamu wote wawe chini ya udikteta wake ni *Riba*. Kwa kutumia Riba atawasababisha binaadamu kuwa masikini wale wote ambao watakuwa wanampinga, na atawapa utajiri na nguvu wale wote ambao watakuwa wanamuunga mkono. Wale matajiri walio tenezezwa kwa njia hiyo atawatumia kama vyombo vyake katika kuwabana kwenye umasikini na kuwanyonya huku wakiwekwa chini ya himaya yake kwa niaba ya huyo Mtume wa uongo.

## SURA YA NNE

# MPANGO MAALUM NA SHIRIKISHO KIYAHUDI-KIKRISTO

Qur'ani imekataza Waislamu kujiingiza kwenye uhusiano wa krafiki au kushirikiana na wale Wayahudi na Wakristo ambao wao wenyewe wanapatana na kuwa na ushirikiano wa Kiyahudi-Kikristo. Qur'ani imetoa tamko hilo katika aya yenye wingi wa msukumo iliyomo katika *Surah-al-Maida* :

Error!

٥١

يَأَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَتَحْذِرُوا إِلَيْهِودَ وَالنَّصَارَىٰ أَوْ لِلَّاهِ بَعْضُهُمْ أَوْ لِيَاءٌ  
بَعْضٌ وَمَن يَتَوَهَّمْ فِنْكُمْ فَإِنَّهُ مِنْهُمْ إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ

“Enyi mlion amini! Msiwafanye Mayahudi na Wakristo kuwa ni marafiki. Wao ni marafiki wao kwa wao. Na mionganini mwenu mwenye kufanya urafiki nao, basi huyo ni katika wao. Hakika Mwenyezi Mungu hawaongoi watu wenye kudhulumu.”

(Qur'ani, al-Maida, 5:51)

Tunaishi haswa kwenye dunia ambayo shirikisho la Kikristo-Kiyahudi limejitokeza kwa mara ya kwanza katika historia tangu dunia ianze. Ni shirikisho hilo ambalo limeunda na kuujenga utamaduni wa kisasa wa

kimagharibi, ambao ndio ambao kwa sasa unatawala dunia kwa kupitia Jumuiya ya Umoja wa Mataifa, n.k. Shirikisho hilo limeunda mfumo wa pesa na mfumo wa uchumi ambayo kwayo imeshawenza kufanikiwa kwa fitna kujitajirisha kwa kuinyonya dunia nzima. Ni shirikisho hilo la Kiyahudi-Kikristo ambalo limeunda Shirikisho la Kimataifa la Fedha (IMF). Msomaji inabidi sasa ajiulize je, aya hiyo ya Qur'ani imekataza kwa Muislamu kujiunga na kuwa mwanachama katika mashirika ambayo yamenundwa na yako chini ya himaya ya Shirikisho hilo la Kiyahudi-Kikristo. Jibu liko wazi.

Matajiri wachache kwa sasa wanawatawala mabilioni ya masikini miongoni mwa binaadamu, na nchi chache tajiri sasa hivi zinatawala mataifa ya dunia yote iliyobaki. Zaidi ya hayo, matajiri hao wachache waliosambaa dunia nzima kwa sasa ni kama jumuiya moja (*Jama'ah*), kwa hivyo jukwaa limeshatayarishwa kwa kuja kwa *Amir*, ambaye ataitawala dunia kutokea Jerusalem naye atakuwa Mtume wa uongo.

Wale ambao hawawezi kumtambua *Dajjal* Mtume wa uongo kama ndiye muunzi na mwanzilishi wa mfumo wa dunia uliopo hivi sasa, kwa sasa anatawala karibu ulimwengu wote wa Kiislamu. Kwa kufanya hivyo wanasababisha kutoweza kufuatwa kwa amri hiyo ya Qur'ani ya kukataza kutokuwa na marafiki na shirikisho la Kikristo-Kiyahudi.

*Wakati wote watu hawa wakiendelea kuwa viongozi wa Waislamu, umma wa Mtume Muhammad (rehma na amani juu yake) wataendelea kuwa wafungwa katika umasikini uliokubuhu na hawatoweza kuupinga na kupigana vita wanayopigwa Waislamu kwa niaba ya taifa la Israel.*

Tunaanza kuelezea moja ya njia za *Riba* ambazo *Dajjal* anawapa nguvu za utajiri wale ambao wanaomuunga mkono na kuwafunga na utumwa wa umasikini wale ambao wanampinga. Alichofanya ni kuunda mfumo wa kimataifa wa pesa ambao umeziharibu pesa kiasi kwamba pesa zinaweza kubadilishwa kiulaghai na kufanywa kuwa chombo halali cha kuibia, kulaghai na ukandamizaji wa kiuchumi. Moja ya njia zilizo wazi ni unyonyaji wa nguvu kazi kwa kulipa mishahara ya kitumwa. Duniani kote, kunakodaiwa kuwa na uchumi unaofuata taratibu za soko huru, serikali zimelazimika kuweka sheria ya kima cha chini cha mishahara ili kuepuka machafuko ya wanaokandamizwa kwa mishahara ya kitumwa, machafuko ambayo yangeweza kusababisha umwagaji wa damu.

Msomaji anaweza kulitambua mara moja chimbuko la uhalalishaji wa mfumo wa kimataifa wa pesa ambao umeundwa na shirikisho la Kikristo-Kiyahudi kwa kukitazama kitendo kilichotokea mnamo mwezi wa nne wa mwaka 1933. Serikali ya Marekani ilipitisha sheria ambayo wakati ule ilikataza raia wake wasiwe na hifadhi ya sarafu za dhahabu, vito vyta dhahabu na nyaraka/vyeti vyta dhahabu katika miliki zao. Vitu hivyo havikuweza kutumika kama pesa. Raia yejote atakayekutwa na dhahabu baada ya tarehe husika, angeweza kutozwa faini ya dola za kimarekani elfu kumi (\$ 10,000) na/au kufungwa jela kwa miezi sita (6). Katika kubadilisha sarafu hizo, Benki Kuu (Federal Reserve Bank), ambayo ni benki inayomilikiwa na watu binafsi, ilitoa pesa za karatasi (noti) zikiwa zimepewa thamani yenye namba ya dola ishirini (\$20) kwa kila aensi moja ya dhahabu.

Wamarekani wengi walikimbilia kubadilisha dhahabu zao na kuchukua pesa za karatasi (noti), lakini wale ambao waligundua udanganyifu unaofanyika

walinunua dhahabu kwa hizo noti na kuzisafirisha kwenda kuzihifadhi katika mabenki ya kiswisi.

Ni muhimu kujua kuwa serikali ya Uingereza ilifanya kitendo hicho hicho mnamo mwaka huo huo kama ilivyofanya serikali ya Marekani.

Waingereza waliziondoa sarafu za dhahabu kwa kusimamisha kubadilishwa kwa noti za pound sterling kwa dhahabu.

Baada ya kubadilisha dhahabu yote kwa pesa za noti, Serikali ya Marekani iliendelea na kupunguza thamani ya noti zake mnamo mwezi wa kwanza ( Januari) mwaka 1934 kwa asilimia 41, na kuiondoa sheria iliyokuwa inakataza raia wake kuwa na hifadhi ya sarafu za dhahabu na vito vingine vya dhahabu kama ilivyopitishwa mwaka mmoja kabla. Wamarekani wakakimbilia tena kubadilisha noti zao za dola na kununua dhahabu kwa bei mpya ya dola 35 kwa kila aensi. Msomaji anaweza kuona wazi jinsi gani wizi unaohalalishwa unavyofanyika wakati pesa inashushwa thamani.

Qur’ani inakataza, na kuita Haramu, wizi wa namna hiyo wa mali za watu. Qur’ani imekataza hayo, kwa mfano kwenye aya za *Sura al Nisa* na *Sura Hud*:

يَأَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَأْكُلُوا أَمْوَالَكُمْ بَيْنَ حُكْمٍ  
بِالْبَاطِلِ إِلَّا أَنْ تَكُونَ تِحْرِرَةً عَنْ تَرَاضٍ مِّنْكُمْ وَلَا نَقْتُلُوْا  
أَنفُسَكُمْ إِنَّ اللَّهَ كَانَ بِكُمْ رَّحِيمًا

“Enyi mlion amini! Msiliane mali yenu kwa dhulma, isipo kuwa iwe biashara kwa kuridhiana wenywewe.....!”

(Qur'ani, al-Nisa, 4:29)

وَنَقُومْ أَوْفُوا الْمِكْيَالَ وَالْمِيزَانَ بِالْقِسْطِ وَلَا تَبْخَسُوا  
النَّاسَ أَشْيَاءَهُمْ وَلَا تَعْثُوا فِي الْأَرْضِ مُفْسِدِينَ



“Na enyi watu wangu! Timizeni vipimo na mizani kwa uadilifu wala msiwakhini watu vitu vyao (kama thamani ya kazi zao, bidhaa, mali, n.k.) wala msieneze uovu katika nchi mkafanya uharibifu.”

(Qur'ani, Hud, 11:85)

Na mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*) pia ametamka kuwa biashara za namna hii zinazofanyika kwa ulaghai na zinazompatia faida au kipato ambacho hakikupatikana kihalali (vitendo vya wizi kwa udanganyifu), kuwa ni *Riba*<sup>2</sup>.

Benki Kuu ya Marekani inaonyesha ilifanya kitendo hicho nyumbani kama ‘majaribio’ ya mfumo mpya wa pesa ambao kwa kuutumia huo mfumo panatokeo uhamishaji mkubwa na usio wa kihalali utajiri wa wakazi wa dunia nzima bila wao kufahamu. Uhamishaji huo unafanywa kwa kutumia kiurahisi kwa kutengeneza pesa za karatasi (noti) zisizokuwa na thamani, na kisha kulazimisha dunia nzima izitumie. Wale ambao wanamiliki na wenye uwezo juu ya mfumo wa pesa duniani wanachofanya baada ya hapo ni kulenga pesa hizo na kuzishusha thamani. Kwa namna hiyo, wakati noti zinashuka thamani

bila kugundua, watu wanapoteza mali zao, hata hivyo ‘kupotea’ kwa mali zao kunasbabisha ‘kuongezeka’ kwa mali za wengine.

Chini ya miaka miwili kabla ya hapo, manmo mwezi wa tisa mwaka 1931, paundi za Kiingereza ailihushwa thamani kwa asilimia 30, nayo ikaongezwa taratibu hadi kufikia asilimia 40 mwaka 1934. Ufaransa ilifuata kwa kushusha thamani ya pesa zake kwa asilimia 30, Lira za Italia zilishushwa kwa asilimia 41 na Fank ya uswisi ilishushwa kwa asilimia 30. Kitu hicho hicho kilitokea katika nchi nyingi za bara la Ulaya. Ugiriki ilivuka viwango vilivyofikiwa na nchi zote kwa kushusha thamani ya pesa zake kwa asilimia 59.

Kilichoonekana kama siasa za “jirani ombaomba” (“beggar-thy-neighbour) za miaka ya 1930, kutumia kushusha thamani ya pesa za nchi husika ili kuongeza mauzo ya nje ya bidhaa zake ili kupunguza uwiano wa upungufu wa malipo- ulisababisha kuanguka kwa kiasi kikubwa sana kipato cha taifa, kupungua kwa matumizi na mahitaji ya bidhaa, kuongezeka kwa kiasi kikubwa kwa ukosekanaji wa ajira na kupungua kwa kiwango cha biashara duniani, kulikokuja kuitwa “Mwanguko Mkubwa wa Uchumi” - “Great Depression.” Hata hivyo, Mwanguko huo, uliutayarishia njia uanzishaji wa mfumo wa pesa wa kimataifa ambao ulidiriki kudai kuwa utaleta utulivu na kukinga machafuko katika dunia ya pesa na biashara. *Kwa maneno mengine, Mwanguko Mkubwa wa Uchumi ulianzishwa kimakusudi kwa ulaghai ili kulazimisha kuanzsishwa na kuwekwa kwa mfumo wa pesa wa kimataifa ambao ungeleta utulivu kwenye dunia ya pesa iliyokuwa imechafuka kwa kukosa utulivu.*

Kitendo hiki kisichokuwa cha kawaida na cha kutia wasiwasi kwa ushirikiano wa nchi za bara la Ulaya katika wakati mmoja wote kwa ulaghai

kushusha thamani ya pesa zao ilipaswa iwaamshe Waislamu juu ya hatari kubwa iliyosababishwa na mfumo wa Kiyahudi-kikristo wa pesa za karatasi.

Shirikisho hili la Kiyahudi-Kikristo liliendelea na kuanzisha mfumo wa pesa za karatsi wa kimataifa uliojadiliwa Bretton Woods. Walitumia kiungo baina ya dola za kimarekani na dhahabu katika makubaliano ya Bretton Woods kama *jani la figi* ili kuficha ukweli kuwa karatasi zingeweza kuanza kuchapishwa na kutumika kama pesa bila ya kujali kama karatasi hizo zinathibitika kwenye soko kama pesa halisi, ikimaanisha pesa zenye thamani ndani ya pesa zenyewe. Mkataba wa Bretton Woods ulifungua njia kwa kuanzishwa kwa SFK - Shirikisho la Fedha la Kimataifa (IMF) mwaka 1944 likiwa na lengo maalum la kusimamia na kuimarisha mfumo wa pesa wa kimataifa wa hizo pesa za karatasi. Hadi mwaka 1971, hata hilo jani la figi lilipotea wakati Marekani ilipokataa kutimiza ahadi yake iliyotoa kwenye mkataba wa kimataifa wa kuithibiti dola za kimarekani kwa dhahabu.

Inashangaza, kwa kweli, kuwa hapakuwa na kipingamizi cha aina yoyote kutoka kwa Wasomi wa Kiislamu kuwahamasisha Waislamu na kupinga mfumo huu mpya wa pesa wa kilaghai. Ikiwa kama Waalimu wa Kislamu walifungwa macho na hilo *jani la figi* ambalo lilikuwa ni dola ya Kimarekani, na hawakuweza kuona hali halisi kuwa mfumo wa kimataifa wa pesa ni ulaghai, pamekuwa hapana jani la figi baada ya mwaka 1971 ambalo limebaki kuficha aibu ya wizi unaohalalishwa. Hata hivyo, Waalimu wa Kiislamu wameshindwa kuona kuwa mfumo wa kisasa wa pesa za karatasi ni *Haramu*. Matokeo yake, ulimwengu wote wa Kiislamu ulifuata shirikisho la Kiyahudi-Kikristo katika kile kinachojulikana kimsemo kama ‘shimo la kenge.’

Wakati shirikisho la bara la Ulaya la Kiyahudi-Kikristo lilipoyaachia makoloni kwa kuyapa uhuru, walihakikisha kuwa nchi zote za dunia zisizokuwa za bara la Ulaya zinamezwa kwa kuwa wanachama wa mfumo mpya wa SFK - Shirikisho la Fedha la Kimataifa (IMF).

Vifungu vya makubaliano ya SFK - Shirikisho la Fedha la Kimataifa (IMF) vinakataza kutumia dhahabu kama pesa.<sup>3</sup> Ilifanya hivyo kwa kutoruhusu kuunganishwa kwa dhahabu na pesa za karatasi zaidi ya (isipokuwa) dola ya Kimarekani. Kifungu cha nne(4), Sehemu ya 2(b) ya Vifungu vya Makubaliano kinasema:

“Mipangilio ya kubadilishana inaweza kujumuisha (i) kudumisha kwa nchi mwanachama kwa thamani ya pesa zake katika hali ya haki maalumu za kutoa pesa au kiigizo kingine, **kisichokuwa dhahabu**, kitakachochaguliwa na nchi mwanachama au (ii) mipangilio ya kushirikiana ambayo nchi wanachama zitadumisha thamani ya pesa zake kulinganisha na thamani ya pesa za nchi zingine, au (iii) mipangilio mingine ya kubadilishana itakayochaguliwa na nchi mwananchama.”

Mwezi wa nne (4) mwaka 2002, mbunge wa Bunge la Wawakilishi (Congress) wa Kimarekani, Ron Paul alituma barua kwenye Wizara ya Fedha na Benki Kuu (ambayo, ni benki inayomilikiwa na watu binafsi) akiuliza swali kwanini Shirikisho la Mfuko wa Pesa la Kimataifa linakataza wanachama wake kutumia pesa zinazothibitishwa kwa dhahabu :

Wapendwa,

Naandika barua hii kuhusiana na Kifungu cha nne(4), Sehemu 2(b) ya Makubaliano ya SFK - Shirikisho la Fedha la Kimataifa. Kama mnavyojua,

lugha hiyo inazikataza nchi wanachama wa SFK (IMF) kuunganisha pesa zao na dhahabu. Kwa kufanya hivyo, SFK (IMF) inazizuia nchi ambazo zina tatizo la kuwa na sera dhaifu za pesa kutumia silaha yenye ufanisi wa hali ya juu kabisa ambayo ni kuunganisha pesa na dhahabu. Sera hii inaweza kusababisha kuchelewesha kurudisha hali bora ya uchumi wa nchi iliyo katika machafuko ya kiuchumu na hivyo kuchelewesha kukua kwa uchumi, hivyo kusababisha udhaifu wa kiuchumi na kisiasa.

Ningefurahishwa sana kupata maelezo ya kina kutoka kwenu nyote: Wizara ya Fedha na Benki Kuu kuhusu sababu zinazoifanya Serikali ya Marekani iendelee kuzisimamia sera hizi potofu. Tafadhali wasiliana na Bwana Norman Singleton, ambaye ni mkurugenzi wangu (wa utunzi) wa sheria, ikiwa utahitaji maelezo ya zida yanayohusiana na ombi hili.  
Ahsante kwa ushirikiano wako katika suala hili.

*Ron Paul*

*Bunge la Wawakilishi la Marekani.*

Ni muhimu kugundua kuwa aidha Benki Kuu wala Wizara ya Fedha hadi sasa hazijajibu na kutoa maelezo juu ya ombi hilo. Sababu inayowafanya washindwe kujibu ni kuwa hakuna maelezo yoyote zaidi ya ukweli kwamba mfumo wa pesa ulianzishwa kuitia Shirikisho la Kimataifa la Fedha (IMF) kwa lengo la kuwanyonya binadamu wote ulimwenguni na hatimaye kusababisha utumwa wa kipesa kwa watu wote ambao shirikisho la Kiyahudi-Kikristo ambalo sasa linatawala dunia limeamua kuwalenga.

SFK - Shirikisho la Fedha la Kimataifa (IMF) lilitumiwa kuanzisha mfumo mpya wa pesa duniani wenye msamiati wa kiajabu na Waislamu wakajikuta wameandamwa na maneno wasiyowahi kuyasikia kabla yake. Tofauti iliyopo baina ya ‘pesa za (karatasi) za ndani’ ambazo zimekubalika kutumika kama chombo cha kubadilishana bidhaa na huduma katika nchi husika, na zile ‘pesa za (karatasi) za nje’ ambazo ni chombo cha kubadilishana bidhaa na huduma nje ya nchi ni kama baina ya “mbingu na ardhi.” Kwa hiyo, ikiwa kwa mfano Waislamu wa Malaysia walitaka kuuza bidhaa kwa Waislamu wa nchi jirani ya Indonesia, Waindonesia iliwabidi watafute ‘pesa za nje’ kulipia manunuzi yao. Hata hivyo, pesa hizo za nje, zilikuwa zimewakilishwa na aidha pesa za karatasi za nchi za Ulaya au dola za Kimarekani. Hivyo, mtego ukawa umeshategwa kujenga soko na mahitaji makubwa ya dola za Kimarekani, kupelekea kuitwa ‘pesa ngumu.’ Wakati wote shirikisho la kiyahudi-Kikristo lilivyoweza kudumisha soko na mahitaji ya pesa zao, kazi yao ilibaki kuhakikisha kuwa wanaendelea kuchapisha pesa hizo, na kwa njia hiyo, kuendelea kuzalisha mali kutoka hewani.

Mpango mbaya uliokuwa ukiusukuma utaratibu wote wa mfumo huo ulikuwa na lengo la kuhakikisha kuwa pesa za nchi za magharibi, na za zile nchi zinazoshabihiana nazo, siku zote zinaongezeka thamani zikilinganishwa na pesa za nchi zilizobaki. Lengo hilo lilitimizwa aidha kwa kampeni za kinyemela au kwa kulazimisha kwa njia ya kushusha thamani ya pesa za nchi zilizobaki. Baada ya kushusha thamani ya pesa hizo, palitokea uhamishaji wa utajiri kwa kiasi kikubwa sana kutoka kwa mamilioni ya watu kuwapa wachache. Hali hiyo ilisababisha pia kwa nguvu kazi kulipwa mishahara ya kitumwa, na ikawafungia wale wote waliochukua mikopo kwenye pesa ngumu kutoka kwa SFK - Shirikisho la Fedha la Kimataifa (IMF) iliyokuwa siku zote tayari kukopesha, ikishirikiana na mabenki ya kibiashara ya Ulaya, kujikuta wana matatizo

yasiyokwisha ya kulipa mikopo ikiwemo nyongeza za asilimia za faida kwa mkopeshaji. Ukweli ni kwamba, mpangilio mzima wa mfumo wa SFK - Shirikisho la Fedha la Kimataifa (IMF) ulianzishwa kwa lengo la kutaka kuwawezesha kufikia matokeo haya. Nchi zilizolengwa, zikajikuta zimenaswa kwenye mikopo mikubwa, zinayosababisha kafilisi utajiri wote wa nchi katika kujaribu kuilipa, huku umasikini ukiongezeka kwani pesa zao zinapoteza thamani siku hadi siku. Haya yote hayakutokea kwa bahati mbaya.

Mwisho, kwa mfano ulio wazi na mbaya kuliko yote, mfumo huu mpya wa kimataifa wa pesa za karatasi umesababisha kuanzishwa kwa mfumo wa benki, ambao umetumia mfumo wa sehemu ya amana (fractional reserve banking) kukopesha kwa tija kutumia pesa ambazo benki hazipo. Hii, pia ilihalalishwa kwa ulaghai. Nina wasiwas i kuwa Mufti wa Kiislamu hawaelewi nini maana ya mfumo wa sehemu ya akiba wa benki (fractional reserve banking) na pia hawana elimu ya kutosha kuhusu historia ya Mfumo wa Kimataifa wa Uchumi ulioelezewa kwa kifupi katika somo hili. Pesa za elektroniki zitakapochukua nafasi ya pesa za karatasi, na mfumo huu usio wa haki utakapokuwa umejitengeneza kuwa bora zaidi, nina wasi wasi kuwa wataamua kuwa pesa za elektroniki pia ni *Halali*.

SFK (IMF) ilianzishwa ikiwa na lengo maalum la kuzuia vikwazo katika kubadilishana kwa pesa ambavyo vingezilinda pesa hizo kulengwa kwa kushushwa kwa thamani zake. Hivyo vifungu vya makubaliano ya SFK(IMF) vinasema kuwa SFK (IMF) “itasaidia katika..... kuondoa vikwazo kwenye kubadilishana kwa pesa za nje vikwazo ambavyo vinazuia kukua kwa uchumi wa dunia.” Kuondolewa kwa vizuizi hivyo katika kubadilishana pesa za nje kutasababisha pesa iliyolengwa kubaki wazi bila kinga kukabiliwa na

mashambulizi ya kipesa ambayo yataisbabishia kuzaliwa kwa faida mporomoko wakati pesa zinapoteza thamani yake.

Mfumo wa Kimataifa wa pesa uliotokana na mukutano wa Bretton Woods umeshafanikiwa kuwafungia mamilioni ya binaadamu kwenye jela ya milele ya umasikini (na wakati mwingine) kwenye ufukara uliokubuhu, wakiwemo watu karibu wote kwenye ulimwengu wa Kiislamu. Hata hivyo, pesa za karatasi zitakapobadilishwa na pesa za elektroniki, hii italeta utumwa wa kipesa. Waislamu inawabidi wawe na majibu yanayopaswa ikiwa wanataka kupata msaada wowote wa Mwenyezi Mungu ambao utawaokoa kutoka kwenye utumwa huu wa kipesa. Majibu hayo ni ya namna gani? Wapi waanz?

## **SURA YA TANO**

### **MAJIBU YETU**

Wakati wowote ambapo Waislamu wanajigundua kuwa wameziacha Sunna za Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*) wakati wanalifuata shirikisho la kiyahudi-Kikristo kuingia kwenye *shimo la kenge*, jibu la msingi ambalo inawabidi walifuate ni kurudi nyuma na kubadili mwenendo na kufanya jitihada ili kuzifuata *Sunna*. Hata hivyo, ikiwa hiyo *Sunna* pia iko kwenye Qur’ani, kama vile ilivyo *Dinari* ya dhahabu na *Dirhamu* ya fedha, hapo inawabidi pia waombe msamaha kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwa kitendo hicho cha kuziacha amri zake na kuharakisha kupata msamaha Wake kwa kujiunga na mapambano ya kupigania kile kilichoachwa. Jinsi gani mapambano hayo yafanywe? Nini wafanye?

#### **Awamu ya Kwanza**

Kutengeneza sarafu za dhahabu na fedha kutawaruhusu Waislamu kutimiza majukumu yao ya kidini kama vile kutoa Zakat, kulipa Mahari na kugharamia Hajj n.k. Zaidi ya hayo, sarafu hizo zitatumika kama ‘hifadhi ya thamani’ na zitawaruhusu matajiri wapate chombo cha kulinda mali zao kuepukana na athari ya kupoteza thamani inayowakuta pale ambapo pesa za karatasi zinashushwa thamani. Kutengeneza sarafu za dhahabu na kuziuza hakutawapatia mamilioni ya masikini na mafukara unafuu, kwani hawatoweza kununua hata *Dinari* moja ya dhahabu. *Hata hivyo, kutengeneza Dinari ya*

*dhahabu na Dirhamu ya fedha na kuziweka katik soko hakika ni kitendo chenye manufaa kwani kitasaidia katika kuendeleza sakata la kuelimisha umma.*

Pale tu wakati sarafu za dhahabu na fedha zitakapoingizwa kwenye mzunguko wa soko na kufanya kazi kama ‘chombo cha kubadilishana’ na pia kutumika kama ‘kipimo cha thamani’ ndipo pesa za *Sunna* zitakapoweza kuwa zimerudishwa kikamilifu. Pesa hizo mara moja zitazibainisha fedha za kilaghai na udanganyifu za karatasi zinazotumika. Kanuni ni kuwa pesa nzuri itaibazibainisha na kuzifichua pesa mbaya. Tunaweza kutarajia kuwa shirikisho la Kiyahudi-Kikristo ambalo sasa linatawala dunia, pamoja na wateja wao kwenye ulimwengu wa Kiislamu, na dunia ya mabenki kwa ujumla, watatumia nguvu zao zote walizonazo kupinga kuingiza na kuanza kutumia sarafu za dhahabu na fedha kama chombo halali cha malipo.

Kwa sababu hiyo, majibu ya msingi ya jumuiya ya Kiislamu kwenye tatizo hili la pesa ni kuelekeza nguvu zote kwenye sheria husika za pesa ambazo zinazuia matumizi ya sarafu za dhahabu na fedha kama chombo halali cha malipo. Umma unabidi uhamasishwe kujiuliza na kuuliza maswali kwanini matumizi ya Dinari ya dhahabu yamezuiwa? Hakuna hata serikali moja duniani itakayoweza kujibu swalii hilo kwa kuwa hata SFK - Shirikisho la Fedha la Kimataifa (IMF) yenye imeshindwa kujibu swalii hilo.

Nguvu za kujibu mashambulizi ya sheria hizo zisizokuwa za haki na za kugandamiza lazima zielekezwe katika namna na desturi inayoshabihiana na mpangilio wa *Sunna* (*Sunna* za mtukufu mtume wetu Muhammad (*rehma na amani juu yake*)). *Sunna* hizo zinatufundisha kuwa katika kupambana ili kujikwamua kutka kwenye makucha ya kugandamizwa kisiasa na kiuchumi,

kitu cha kwanza kufanya ni mpango wa kuelimisha umma. Somo hili limeandikwa hususan kwa kutimiza lengo hilo.

Hata hivyo, Waislamu wengi hawawezi kukubali kuwa pesa zinazotumika hivi sasa ni za kilaghai na mfumo mzima wa pesa ni udanganyifu na uonevu ikiwa Umma wenyewe haulielewi somo hilo vilivyo na wanabaki katika kuutetea mfumo huo usio halali na Haramu. Huenda ikawa bora kuwakumbusha waislamu kuwa mtume wetu Muhammad (*rehma na amani juu yake*) alionya kuwa utafika wakati ambapo maulamaa wa Kiislamu watausaliti Uislamu kiasi kwamba watakuwa mionganoni mwa “watu wabaya kuliko wote ulimwenguni (chini ya mbingu)” na “hakuna chochote kitakachobaki katika Uislamu isipokuwa jina la Uislamu”:

“Hautapita muda mrefu kabla haujafika wakati ambapo hauna kitakachobaki katika Uislamu isipokuwa jina, na hakuna kitakachobaki katika Qur’ani isipokuwa (vipande vipande vy) maandishi. (Wakati huo) Misikiti yao itakuwa ya majengo makubwa isipokuwa hawatakuwa na Mwongozo, Na (wakati huo) Ulamaa wao watakuwa watu wabaya kuliko watu wowote chini ya mbingu. Kutoka kwao (hao Ulamaa) kutapatikana Fitnah na kwao itawarudia.”

(Sunna, Tirmidhi)

## **Awamu ya pili**

Awamu ya pili ya mapambano itajumuisha kukataa kwa vijiji nje ya miji mikubwa kukataa kupokea na kutumia pesa za karatasi au pesa za elektroniki. Wakulima wa mpunga wa kisiwa cha Java cha Indonesia kwa mfano, watahamasishwa kuwa walipwe kwa kutumia Dinari za dhahabu. Ikiwa wanunuzi watakataa kulipa kwa kutumia Dinari, wakulima wanaweza kutumia mchele wao kama pesa kwa kuutumia mchele kama chombo cha kubadilishana na kununulia na kulipia bidhaa na huduma. Hivyo mchele utatumika kama pesa. Matumizi ya mchele kama pesa yatakuwa ni kitendo cha muda mfupi na huenda ikawa ni kwa ajili ya manunuzi na uuzaji wa vitu vidogo vidogo. Kwa njia hii, pesa za Sunna zitachukua nafasi ya pesa za karatasi na pesa za elektroniki japo kwenye kununua na kuuza bidhaa au huduma za bei ndogo.

Miji itabaki kwenye mtego wa pesa za elektroniki kwa muda wote ambao utawala wa Gog na Magog utaendelea kushika hatamu duniani<sup>4</sup>. Hata hivyo, pesa za Sunna zinaweza kuendelea kusambazwa kwenye matumizi kutoka vijijiini kuja mijini hadi pale utabiri wa mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*) utakapotimia:

“Abi Bakr ibn Abi Maryam aliripoti kuwa amemsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu akisema: “Kwa hakika muda utawafikia binaadamu ambapo hapatokuwa na chochote (kilichobaki) ambacho kitakuwa na matumizi (yenye manufaa) ukiondoa *Dinari* na *Dirhamu*.”

(Musnad, Ahmad”)

**Mwisho**

## Vielelezo

<sup>1</sup>Qur’ani imeweka na kusisitiza kimsingi tofauti kati ya ‘biashara’ na ‘kukopesha pesa’. Katika kila tendo la biashara lazima pawepo na kujihusisha na kipengele cha uwezekano wa kupata faida au (hatari) ya kupata hasara. Mwenyezi Mungu ndipo anapoweza kuingilia kati na ‘kuchukua’ kutoka kwa mmoja na ‘kutoa’ kumpa mwingine. Kwa njia hii, Yeye mwenyezi Mungu, Mtukufu, atahakikisha kuwa utajiri unazunguka katika uchumi mzima. Matajiri hawatoweza kubaki matajiri wakati wote na masikini hawatobaki kuendelea kufungwa jela ya masikini kwa muda wote.

Wakati pesa inakopeshwa kwa malipo ya maslahi ya asilimia ya pesa yenye we inayokopeshwa kama ziada, mkopeshaji anajikinga na uwezekano wowote ule wa kupata hasara. Kwa sababu hiyo, pesa hazizunguki kwenye uchumi unaoendeshwa kwa malipo ya Riba. Matajiri wanaendelea kuwa matajiri na masikini wanaendelea kubaki masikini na rahisi kuendela kunyonywa.

Wananwake wanyonge wa Kiislamu kutoka vijijini Indonesia, kwa mfano, inawabidi wafanye kazi kama watumishi majumbani mwa watawala wasio Waislamu wa Singapore, bila kujali kuwa waajiri wao hawaupendi Uislamu. Pamoja na kulazimika kupika, kutayarisha na kutenga mezani nyama za nguruwe, inawabidi pia wafanye kazi masaa 24 kila siku bila mapumziko siku zote nah ii yote kwa malipo ya kitumwa.

<sup>2</sup>“Anas ibn Malik aliripoti kuwa mtume wa Mwenyezi Mungu alisema: Kumdhulumu mtu (ye yote ambaye hajui bei kamili ya bidhaa yake sokoni-mustarsal) ni Riba.”

(Sunan Baihaqi)

“Abdallah bin Abu Aufa aliripoti: Kulikuwa na mtu aliyepanga bidhaa zake sokoni na akaapa kwa uwongo kuwa ameahidiwa kulipwa kiasi kadhaa cha pesa kwa bidhaa zake ingawa hakupewa ahadi hiyo: Hakika! Wale wote wanaonunua kwa faida kidogo kinyume na amri ya Mweneyezi Mungu na viapo vyao.... watapata adhabu chungu. (3:77) Ibn Abu Aufa akaongeza: Mtu huyo (kama alivyoelezwa hapo juu) ni mlaji wa Riba aliye msaliti.”

(Bukhari)

Biashara zote zinazofanywa kwa udanganyifu kama vile kuficha bei kamili ya soko, zinaweza kusababisha muuzaji au mnunuzi kuuza au kununua bidhaa au huduma kwa bei ya juu au ya chini kuliko bei ya soko, na hivyo aidha kupata faida au au faida kubwa zaidi kuliko ile ambayo angeipata kihalali. Tunaweza kufikia uamuzi kuwa kitendo chochote cha biashara iliyofanywa kwa udanganyifu na kumletea mhusika faida kubwa zaidi ya ile ambayo angeipata kihalali kama angeuza bidhaa au huduma yake kwa bei halali ya soko, ni *Riba*. Mfumo wa kisasa wa pesa unaotegemea pesa za karatasi zisizothibitika ambazo siku hadi siku zinashushwa thamani ni mfanommojawapo wa udanganyifu ambao unawapatia faida au mapato ambayo hao waanzilishi wa mfumo huo hawapati kihalali. Hivyo hiyo nayo lazima iwe ni *Riba*.

<sup>3</sup>Msimamizi wa mtandao wa mwandishi huyu amemfahamisha kuwa kuna mtu ndani ya SFK - Shirikisho la Fedha la Kimataifa (IMF) ambaye amekuwa mara kwa mara akiitembelea tovuti ya mwandishi huyu, na mwandishi anaikaribisha SFK (IMF) kumsawazisha katika jambo hili kama anakosea.

<sup>4</sup>Kuna sura nzima na kamili katika Kitabu ‘Jerusalem katika Qur’ani’ ambayo inaelezea kuhusu suala la Gog na Magog katika Uislamu.